Fomu ya maombi: Tuzo ya Liz Hughes kwa vituo vya redio vinavyohamasisha usawa wa kijinsia

Tuzo hii inatambua vituo vya redio, watangazaji na waandaaji wa vipindi waliojitoa kuwahudumia wanawake wanaosikiliza vipindi vya redio. Vipindi ambavyo vinazungumzia haki sawa na usawa wa kijinsia kwa kina. Vipindi ambavyo Vinazungumzia uzoefu na mawazo ya wanawake au masuala yanayowahusu wanawake. Shirika la Kimataifa la Redio kwa Wakulima(Farm Radio International) hutoa tuzo hii kama kumbukumbu ya mjumbe wa Bodi Liz Hughes.

Vijiji vya nchi zilizo Kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika, wanawake hufanya shughuli zenye umuhimu mkubwa za kilimo kwenye familia na jamii. Japo wao ndio waathirika wakubwa wa umasikini, utapiamlo na afya dhaifu.Pia wana uwezekano mdogo wa kupata na kudhibiti rasilimali, pamoja na habari. Ni muhimu kwa vituo vya redio kurusha vipindi vinavyowasidia katika kukidhi mahitaji na matakwa ya wanawake pamoja na wanaume. Kwa namna hii,wanawake na wanaume wote wanaweza kunufaika na taarifa zinazotolewa redioni na kuchangia katika maendeleo ya jamii.

Jifunze zaidi kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia kwenye haki za ardhi kwenye utangulizi huu. Jifunze zaidi kuhusu jinsi ya kuwahudumia vizuri wakulima wanawake kwenye muongozo huu wa watangazaji.

Timu ya utangazaji itakayoshind itapokea cheti na tuzo ya CAD $ 1,000 kwa kutambua kazi yao nzuri.

Vigezo:

Kituo chochote cha redio Kusini mwa Jangwa la Sahara kinaweza kuomba tuzo hii. Tuzo hii ni ya kituo cha redio / timu ya programu na watangazaji / mameneja wa kituo wanapaswa kuwasilisha kwa niaba ya timu. Vituo vinaweza kuwasilisha maombi zaidi ya moja ikiwa inaomba kwa niaba ya mipango tofauti.

Kumbuka: "Programu" inahusu programu kwa ujumla, na "kipindi" kinamaanisha matangazo ya kibinafsi (kila wiki au ya kila siku) ya programu. Tafadhali usiwasilishe maombi ya vipindi vingi. Tumia kipindi chako bora kama mfano katika programu, lakini sehemu moja tu kwa kila mpango itakubaliwa.

Waombaji wanaombwa kupeleka rekodi ya programu yao na maombi yao ili tuweze kusikia ubora. Tafadhali chagua kipindi kilichotangazwa mnamo 2021. Tunaelewa kuwa vipindi vinatangazwa katika lugha nyingi za hapa. Tafadhali toa nakala ili tuweze kuelewa kile kinachojadiliwa katika kipindi hicho.

Washindi wa zamani wanaalikwa kuwa sehemu ya majaji kwa tuzo hii na kwa hivyo hawastahiki kuomba kwa miaka 5 baada ya ushindi wao.

Tarehe ya mwisho ya kuomba ni Oktoba 1, 2021. Tuma fomu yako ya maombi, safu ya programu, na kipindi kilichorekodiwa kwa barua pepe radio@farmradio.org

Maombi yatakubaliwa kwa Kiingereza, Kifaransa, Kiamhariki, Kiswahili, na Kihausa. Kurekodi kipindi kunaweza kuwa katika lugha ya matangazo. Tafadhali toa muhtasari wa kipindi.

Taarifa za kituo:

Jina la kituo: _____

Nchi: _____

Mkoa/Mji: _____

Barua pepe: _____

Namba za simu: _____

Taarifa za Kipindi:

Jina la Kipindi: _____

Mada ya kipindi: _____

Urefu wa kipindi: _____

Muda wa kipindi: _____

Taja majina ya wafanyakazi wote wanaohusika kuandaa na kurusha kipindi, pamoja na jinsia zao. Hawa wanaweza kuwa ni Meneja, waandaaji, watangazaji, waandishi, mafundi mitambo.

Jina	Kazi	Jinsia (Me/Ke)

Tafadhali weka kiambatanisho kinachoonyesha mtiririko wa kipindi

Maombi:

1. **Nini lengo la kipindi?** Je wasikilizaji wako wakuu ni nani, na wana sifa gani kuu?

2. **Je unashughulikiaje swala la usawa wa kijinsia? Je unaboreshaje uelewa wa wasikilizaji kuhusu usawa wa kijinsia? Tafadhali tuambie ni mada zipi unazojadili.** Tafadhali tuambie kindi chako kinashughulikiaje haki za wanawake,nafasi ya wanawake katika kufanya maamuzi pamoja na wanawake kupata na kumiliki taarifa.

3. **Je kipindi hiki kinawahudumiaje wanawake wasikilizaji?Je! Unahakikishaje kuwa kipindi chako kinazungumzia majukumu ya wanawake?** Je unaweza kuelezea kisa chochote cha imani potofu ya kijinsia na jinsi kipindi chako kilivyoweza kufundisha ili kuachana na hiyo dhana potofu. Kwa mfano, unazungumza kuhusu wanaume na wanawake katika majukumu yasiyo ya kitamaduni? Je huwa unazungumzia kuhusu wanawake kuzalisha mazao ya biashara , wanawake kuwa mstari wa mbele/viongozi, au mchango wa wanaume kuhusu maswala ya afya na lishe?

4. **Je unahakikishaje kuwa unaandaa kipindi kinachokidhi kufikia malengo ya usawa wa kijinsia?** Tafadhali eleza jinsi unavyojumuisha mwanamke na maswala ya wanawake katika kila hatua unapopanga na kuandaa kipindi chako. Kwa mfano, wanawake wanahusika vipi katika hatua ya maandalizi. Je unakuwa na mwanamke mtangazaji, Je unawahusiha wanawake wataalam kwenye kipindi chako, Je unashirikisha Shirika lolote la wanawake kwenye maandalizi ya kipindi chako?

5. **Elezea jinsi ambavyo sauti au maoni ya wanawake na wasichana yanavyohusishwa kwenye kipindi. Jisikie huru pia kuweka mifano jinsi unavyoshirikisha wanaume katika kuzungumzia usawa wa kijinsia.***(Kwa mfano: kupitia vox pops, mahojiano kwenye redio,mijadala, maswali na majibu kupitia Uliza, mahojiano na wataalamu, mahojiano yaliyorekodiwa nk.*

6. **Je ni changamoto gani ulikumbana nazo wakati wa kuandaa kipindi hiki ? Je, ulikabilianaje nazo ?**
   Kama inawezekana,tafadhari tumia mfano unaonyesha jitihada zako katika kutetea maswala ya kijinsia. Kwa mfano, inakuwa changamoto kuwahusisha wanawake katika kipindi cha redio? Je unapata ugumu kuwapata wanawake wataalamu kushiriki kwenye mahojiano? Je, umepata ugumu wowote katika kuzungumzia masuala au mada nyeti kwenye kipindi kikiwa hewani?

7. **Je ni jinsi gani kipindi hiki kimeleta mabadiliko ya usawa wa kijinsia kwenye eneo lako? Elezea mabadiliko yoyote katika jamii yako tangu ulipoanza kurusha kipindi hiki.** Ikiwezekana, toa mifano jinsi usawa wa kijinsia unavyoboreshwa katika mkoa wako.Kwa mfano, ni mrejesho gani uliopata kutoka kwa wasikilizaji wa kipindi? Je kumekuwa na matokeo yoyote katika ngazi ya kaya na jamii kwa ujumla? Je, kumekuwa na badiliko lolote katika majukumu au shughuli anazofanya wanawake? Je kuna majadiliano yoyote yaliyowahi yaliyofanyika?

8. **Ni lazima *uambatanishe na kipindi chako kilichorushwa ndani ya mwaka 2021 kilicho kwenye mfumo wa MP3***. Tafadhari ambatanisha na *muhtasari mfupi wa kipindi hicho, tunaelewa kuwa labda unatangaza katika lugha yako. Tafadhali jumuisha mada zilizojadiliwa, ni nani aliyehojiwa, na maoni yaliyotolewa. Haya ni muhimu kwani vigezo vyetu kwa ajili ya tathmini.*